TANGAZO LA SERIKALI NA. 942.la tarehe 29/11/2019

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA,

(NA. 5 YA MWAKA 2019)

AGIZO

(Imetolewa kwa mujibu wa kifungu cha 29(1) (d))

AGIZO LA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA BIHARAMULO (BIHARAMULO WSSA), LA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA), 2019

Jina la Agizo

1. Agizo hili litajulikana kama, Agizo la Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Biharamulo(Biharamulo WSSA), (la Kurekebisha Bei za Huduma za Maji safi), la Mwaka 2019.

Tarehe ya Kuanza

2. Agizo hili litaanza kutekelezwa rasmi kuanzia tarehe 1 Disemba 2019.

Marekebisho ya Bei

3. Bei za majisafi na usafi wa mazingira za Biharamulo WSSA zinarekebishwa kulingana na Jedwali la Kwanza katika Agizo hili.

Masharti

4. Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo:

(a) kabla ya kuanza kutekeleza bei mpya, Biharamulo WSSA iwasilishe EWURA vielelezo kwamba ilitoa taarifa kwa wateja wake kuhusu bei mpya za huduma zake na pia ilitoa elimu kikamilifu kwa umma ikiwa ni pamoja na wawakilishi wa wananchi, serikali na viongozi wa dini katika eneo lake la huduma;

(b) Biharamulo WSSA ihakikishe inanunua na kuweka stoo dira za kutosha kwa ajili ya kubadilisha zilizokwisha muda wake ili zoezi la ubadilishwaji wa dira lifanyike kwa kipindi kifupi kadri iwezekanavyo;

(c) Biharamulo WSSA, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza

miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Agizo hili;

(d) Biharamulo WSSA itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Tatu la Agizo hili;

(e) Ifikapo tarehe 31 Januari 2020 au kabla, Biharamulo WSSA itawasilisha EWURA Mpango wake wa Kibiashara (2019/20-2021/22) uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Agizo hili;

(f) Biharamulo WSSA itahakikisha inalipa tozo ya udhibiti ya EWURA;

(g) Ifikapo au kabla ya tarehe 31 Januari 2020, Biharamulo WSSA itatengeneza na kuituma EWURA mpango wa kuainisha wateja wenye uwezo duni katika eneo lake, na kuwapatia huduma za maji katika mtindo nafuu;

(h) Ifikapo tarehe 31 Januari 2020 au kabla Biharamulo WSSA iandae na kuwasilisha EWURA mpango wa kuwafikia wateja wake kwa lengo la kutoa elimu juu ya Huduma za maji;

(i) Biharamulo WSSA, kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Agizo la Bei na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa kama yalivyoainishwa katika Jedwali la Nne la Agizo hili;

(j) Biharamulo WSSA ihakikishe vitabu vyake vya fedha vinakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali au mtu yeyote ambaye ameidhinishwa kama inavyobainishwa katika kifungu cha 33(1) cha Sheria Ukaguzi wa Hesabu za Umma na kuwasilisha nakala EWURA; na

(k) Biharamulo WSSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA, taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Biharamulo WSSA ikilinganishwa na Mamlaka nyingine za majisafi na Usafi wa Mazingira na uboreshaji wa huduma zake. Pia EWURA itazingatia tathmini hii katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na

Biharamulo WSSA katika siku zijazo

Utenguzi wa T.S. Na 40 la 2018

5. Agizo hili linatengua Agizo la Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Biharamulo (Biharamulo WSSA) Tangazo la Serikali la mwaka 2018.

_____

MAJEDWALI

_____

JEDWALI LA KWANZA
BEI, ADA NA TOZO ZILIZOIDHINISHWA
(Limetengenezwa chini ya aya ya 3)

Jedwali 1.1: Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi/ Mita ya Ujazo)

Kundi la Wateja	Matumizi ya Maji ya sasa	Bei ya Sasa	Bei zilizoidhinishwa		
		2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Majumbani	1--5	1,220	1,300	1,310	1,350
	6--10	1,280	1,360	1,370	1,420
	>11	1,300	1,380	1,390	1,440
Taasisi		1,530	1,630	1,640	1,700
Biashara		1,560	1,660	1,670	1,730
Viwanda		2,000	2,000	2,000	2,000
Magati		1,500	1,500	1,500	1,500
Wastani wa Bei Linganifu		1,200	1,300	1,300	1,400

Jedwali 1.2: Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Maunganisho Mapya (TZS/Maunganisho)

Kundi la Wateja	Ada za Sasa	Ada Zilizoidhinishwa		
		2019/20	2020/21	2021/22
Majumbani	Asilimia 20 ya gharama za maunganisho mapya ya maji kama ilivyobainishwa katika kifungu cha 24(3) cha Kanuni za Maji za Mwaka 2013	Asilimia 20 ya gharama za maunganisho mapya ya maji kama ilivyobainishwa katika kifungu cha 24(3) cha Kanuni za Maji za Mwaka 2013		
Taasisi				
Biashara				
Viwanda				
Magati				

Jedwali 1.3: Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Marejesho ya Huduma ya Maji Baada ya Kukatiwa (Shilingi/Kurejeshewa Huduma)

Kundi la Wateja	Ada za Sasa	Ada Zilizoidhinishwa		
		2019/20	2020/21	2021/22
Majumbani	20,500	15,000	15,000	15,000
Taasisi	21,500	15,000	15,000	15,000
Biashara	21,000	15,000	15,000	15,000
Viwanda	-	15,000	15,000	15,000

JEDWALI LA PILI]

(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(c))

MIRADI ITAKAYOTOKELEZWA (SHILINGI ZA KITANZANIA)

Maelezo ya Kazi Zitakazotekelezwa	Kipindi cha Utekelezaji		
	2019/20	2020/21	2021/22
Kununua na Kuweka dira za maji 571 zenye kipenyo cha milimita 20 za daraja C kwa wateja wapya ifikapo Juni 2022	8.50	10.50	21.00
Kununua na kubadilisha dira 50 zilizochakaa ifikapo Juni 2021	-	3.51	-
Upanuzi wa mtandao wa maji kwa urefu wa km 7 kwa OD 63mm katika maeneo ya Ng'ambo na Nyakantutu ifikapo Juni 2020	59.61	-	-
Kununua pikipiki mbili ya aina ya boxer, cc 150	-	3.00	3.35
Kununua na kusimika pump ya 60m3/hr ifikapo June 2022	-	50.00	50.00
Jumla ya Gharama ya Miradi	68.10	67.01	74.35

JEDWALI LA TATU

(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(d))

VIASHIRIA VYA UTENDAJI (2019/20 – 2021/22)

Maelezo ya Viashiria	Uniti	Lengo la Utendaji		
		2019/20	2020/21	2021/22
Idadi ya maunganisho mapya ya majisafi	Na	250	275	315
Ufungaji wa Dira	%	100	100	100
Upotevu wa Maji	**%**	18	18	14
Ufanisi wa ukusanyaji wa mapato (bila malimbikizo ya madai)	%	96	98	98
Wastani wa Saa za Huduma	saa	15	16	18

JEDWALI LA NNE

(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(i))

GHARAMA ZILIZOIDHINISHWA (SHILINGI KATIKA MILIONI)

Aina ya Gharama	2019/20	2020/21	2021/22
Uzalishaji Maji	42.68	49.08	58.90
Umeme kwa ajili ya Uzalishaji maji	142.54	163.93	196.71
Usambazaji Maji	29.60	43.00	58.30
Matengenezo	126.00	138.00	179.00
Watumishi	50.19	82.34	104.06
Utawala	38.98	41.89	45.71
Matangazo	1.00	1.05	1.09
Matukio	4.90	5.04	5.98
Bodi	8.58	9.00	19.30
Fedha	0	0	0
Jumla ya Gharama za Uendeshaji	444.47	533.32	669.05
Uchakavu	68.16	67.01	74.35
Jumla ya Mahitaji ya Fedha	512.63	600.33	743.45
Ondoa Mapato Mengine yasiyotakana na Mauzo ya Maji	19.67	28.28	32.92
Mahitaji ya Fedha Yanayotokana na Mauzo ya Maji	492.96	572.05	710.53

Dodoma
14 Novemba, 2019

NZINYANGWA E. MCHANY
Mkurugenzi Mkuu